JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu:
Mkuu wa shule
0712500071/0755854233
Makamu Mkuu wa Shule
752984655/0621000577
Matron 0716830898

Shule ya Sekondari ya
Wasichana Bunge,
S.L.P 1060,
Dodoma.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....
.....
S.L.P.....
.....

Ndugu,

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BUNGE; HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA MKOA WA DODOMA MWAKA 2021**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2021 tahasusi ya ..... Shule ya Sekondari ya wasichana Bunge ipo umbali wa kilometa 40 mashariki mwa mji wa Dodoma.
   Unapanda basi la Chamwino katika kituo cha mabasi cha Sabasaba, nauli ni shilingi 1500/ mpaka njia panda ya Kikombo. Unashuka na kupanda pikipiki kwa shilingi 3000 mpaka shuleni.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/07/2021. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 03/07/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 01/08/2021.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**
   2.1 Sare ya shule ya darasani

a) Kwa wasio waislam:
   (i) Shati mbili nyeupe za mikono mirefu.
   (ii) Sketi mbili (2) ndefu zinazofunika magoti zenye miraba dark blue na myeupe na marinda 13-15 yanayoangalia upande mmoja yaliyolingana.
   (iii) Koti jeupe lenye michirizi (strips) ya kitambaa cha sketi mikononi na kwenye kola, kama inavyoonekana kwenye picha.
   (iv) Bedge ya nembo ya taifa.

**N.B Sare hii ya darasani itapatikana shuleni kwa wale watakaoshindwa kuipata**
   (v) Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
   (vi) Soksi jozi mbili nyeupe ndefu hadi magotini.



Scanned with CamScanner

(vii) Sweta mbili (2) zenye rangi nyeusi na shingo ya V

(viii) Tai 2 ndefu zenye rangi ya kitambaa cha sketi.

(ix)T-shirt ya rangi ya kijivu yenye kola (form six) iliyo na nembo ya shule (Itapatikana shuleni).

(x) Wanafunzi wote wanatakiwa kunyoa nywele

MUHIMU:

b) Kwa waislam wanaofunika kichwa:

- Aje na hijab (juba) ni nyeupe isiyo na urembo, ndefu hadi kifuani na **HARUHUSIWI KUSUKA.**
- Sketi ya darasani iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu.

2.2. Sare nyinginezo za shule

Wanafunzi wote watatakiwa kuja na:-

- ✓ Magauni mawili (2) ya solo, marefu yanayofunika kifundo cha mguu kilicho karibu na nyayo kwa ajili ya kushindia (shamba dress) ya kitambaa kizito cha rangi ya damu ya mzee (maroon)
  - Solo isiwe pana sana.
- ✓ T-shirt ya michezo, nyeupe yenye shingo ya mviringo.
- ✓ Jezi nyeupe yenye michirizi (strips) myeusi isiyo na kola.



Scanned with CamScanner

- ✓ Sare ya michezo; track suit ya dark blue yenye mistari (strips) myeupe pembeni
- ✓ Raba nyeupe.

**Mwanafunzi asafiri na sare ya shule aliyotoka kama hajapata sare rasmi ya shule hii, kwa wale ambao watakuwa hawajashona.**

**Nguo za nyumbani, haziruhusiwi; akija nazo zitateketezwa na mwanafunzi atarudishwa nyumbani mara moja endapo atakiuka kipengele hiki.**

## 3. MICHANGO NA MAHITAJI MUHIMU:-

a) Ada

Wanafunzi wote watatakiwa kulipa ada (sh. 70,000/= kwa mwaka au 35,000/= kwa muhula mmoja) kwenye; **BUNGE GIRLS SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCOUNT** Na. **015051618500** katika benki ya **CRDB** (Tafadhali andika **jina la mwanafunzi na kidato chake** kwenye pay-in slip).

b) Michango mingine:-

i. Shilingi 15,000/= kukodisha godoro kwa mwaka (isiwe lazima)
ii. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza (Wanafunzi washauriwe kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya ama ikiwezekana ni vizuri awe na NHIF (anaweza kusaidiwa kujiunga akiwa hapa shuleni)
iii. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)
iv. Shilingi 30,000/=kwa ajili ya taaluma.
v. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
vi. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
vii. Shilingi 2,000/= nembo ya shule.
viii. Shilingi 25,000/= Mitihani ya kujipima mock

**Angalizo**: Jumla ya ada na michango ni 193,000/=

c) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i. Mwanafunzi anatakiwa aje na Tsh. 10,000/= kwa ajili ya ream 1 ya karatasi (kwa mwaka) na Tsh. 2,000/= ya graph pad.
ii. Fedha ya badge (beji) ya bendera ya Tanzania Tsh. 3,500/=
iii. Mwanafunzi anashauriwa kuja na hela kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya masomo ya tahasusi husika baada ya kupata ushauri wa mwalimu wa somo husika.
iv. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
v. Scientific calculator (hasa fx 991 ama 992)
vi. Godoro atapata shuleni kama ilivyooneshwa kipengele **(3b(i))**
vii. Mashuka jozi 2 (pinki) na foronya endapo anatumia mto.
viii. Blanketi 1
ix. Chandarua 1 **nyeupe** yenye ukubwa wa futi 3 au 4 ya pembe nne.
x. Taulo na jozi moja ya khanga/kitenge



Scanned with CamScanner

xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli,na kikombe **visiwe vya plastiki**, kijiko na chombo safi cha kuhifadhia maji ya kunywa.

xii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko

xiii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mfagio wa ndani 1 na mfagio wa nje 1.

xiv. Aje na sabuni za kuogea na kufulia, mswaki na dawa ya meno, mafuta ya kupaka/losheni, taulo za kike (pedi), skin taiti, sidiria na chupi za kutosha. **Nguo zote za ndani ziwe za rangi nyeupe au pink tu**

xv. Sanduku la chuma (tranka), tochi na betri zake/ tochi ya sola.

## 4. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya **siku 90 bila taarifa** / utoro.

(iii) Kugoma au kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa jumla.

(v) Kupigana; mwafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.

(vi) Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(viii) Uvutaji wa sigara.

(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.

(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi

(xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xiv) Kudharau bendera ya Taifa.

(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 5. Viambatisho na Fomu Muhimu

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. (imeambatishwa ukurasa wa 6)

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai. (mkataba huu utapatikana shuleni)

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (imeambatishwa ukurasa wa 5)

d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu



Scanned with CamScanner

**MUHIMU**

6. Baada ya kupakua (download) fomu hii, tafadhali jaza jina la mwanafunzi, anwani yako pamoja na tahasusi aliyochaguliwa kusomea hapa Sekondari ya wasichana BUNGE. Hakikisha unajaza **tahasusi (combination) aliyopangiwa na serikali**.
   Taarifa hizi zijazwe kwenye ukurasa wa kwanza.
7. Mwanafunzi atakaporipoti shuleni aje na fomu hii pamoja na result slip ya kidato cha nne.
8. Tafadhali **soma kwa makini** maelezo /maagizo haya na **kuyatekeleza kikamilifu.**
9. Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya kama anayo.

**KARIBU SANA BUNGE SEKONDARI**

SALOME ELIA MKOMBOLA

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMISTRESS
BUNGE GIRLS HIGH SCHOOL
P. O. Box 1060
DODOMA



Scanned with CamScanner

***OR – TAMISEMI***
***HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA***

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BUNGE**
**FOMU YA KUKUBALI SHULE**

## A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi (Majina kamili) ……
   Nimekubali kuingia kidato cha …… katika Shule ya Sekondari ya wasichana BUNGE - Dodoma kuanzia tarehe …… hadi nitakapomaliza kidato cha ……
2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki ka shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.
3. Tarehe ya kuzaliwa…… Kijiji……
   Tarafa…… Wilaya …… Shule unakotoka ……Namba yako ya mtihani……
4. Kituo cha gari (Bus) au Gari la Moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako……
5. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ……

Sahihi ya mwanafunzi …… Tarehe ……

## B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi (majina kamili) …… ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari ya Wasichana BUNGE kuanzia kidato cha ……hadi atakapomaliza kidato cha ……. Nakiri kukubaliana na sheria,kanuni,kulipa ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
2. Jina kamili la Mama …… Jina kamili la Baba……
3. Kazi ya Mama ……Kazi ya Baba ……
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi ……
   ……
5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaishi hapa Dodoma na wanaweza kumsaidia wakati wa dharura( picha zao)

| Jina kamili | Mahusiano | Anakoishi | Simu yake |
|---|---|---|---|
| (i)…… | …… | …… | …… |
| (ii)…… | …… | …… | …… |
| (iii)…… | …… | …… | …… |
| (iv)…… | …… | …… | …… |

6. Madhehebu ya Dini ya Mtoto ni Lutheran/Katoliki/Anglican/PAG/TAG/ Moravian /SDA/Mwislam
7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa ……
   ……

Saini ya Mzazi/Mlezi …… Tarehe ……



Scanned with CamScanner

## *BUNGE SECONDARY SCHOOL*

## *FORM FOR STUDENTS MEDICAL EXAMINATION*

***To be completed by a Medical Officer***

..... (Insert name of the Government Medical Institution)

Name of Student ..... Form ..... Year.....

Age.....Sex.....

Blood count.....

Stool .....

Urine .....

T. B. Test.....

Eyes.....

Ears.....

Chest.....

Spleen .....

Abdomen.....

Teeth .....

Additional information: - (*e.g. pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic or family diseases).*

.....

.....

.....

**I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School for two years.**

Name of Medical Officer ..... Signature .....

Designation .....

Station & Official Stamp..... Date .....

***Sharti mtoto apimwe kikamilifu kabla ya daktari kujaza fomu hii. Ikigundulika kuwa daktari alijaza fomu hii bila vipimo kufanyika, wahusika watachukuliwa hatu za kisheria na za ukiukaji wa haki za binadamu.***



Scanned with CamScanner